**Kuzimu ni Halisi, nilikwenda huko!**

na Jennifer Perez

*Ushuhuda wa msichana mwenye umri wa miaka 15 ambaye alilelewa katika Familia ya Kikristo. lakini baadaye alirudi nyuma katika safari yake ya wokovu, alijikuta akitumia madawa ya kulevya kupindukia, akafa, na kupelekwa Kuzimu. Kwa neema tu, alipewa nafasi ya pili na mpango/ ujumbe wa haraka wa kuja tena na kuonya waliovuguvugu na waliopotea,*




***www.DivineRevelations.info/SWAHILI***

Mungu akubariki kaka na dada, ningependa ufungue Biblia yako na urejee Yoeli 2:28 *"Na baada ya hayo, nitamimina Roho yangu juu ya watu wote wana wenu na binti zenu. watatabiri, wazee wenu wataota ndoto, na vijana wenu wataona maono. "*

Jina langu ni Jennifer Perez na mimi nina umri wa miaka 15. Ni vigumu kwa kijana kama mimi kuja kwenu na kutambua/kukiri makosa yangu mwenyewe. Lakini kwa msaada wa Roho Mtakatifu, Yeye atanisaidia, na kunipa mimi nguvu ninazohitaji. Awali ya yote nataka kusema kwamba hii ni kwa Heshima na Utukufu wa Bwana wangu Yesu Kristo. Sitaki kusema fundisho/msingi au kuweka fundisho/msingi mpya, ninakwenda tu kuwaambia kile nilichokiona, nikasikia, na kukihisi.

Ningependa kukuambia kidogo kuhusu familia yangu. Wazazi wangu ni Wakristo, na wao daima wamekuwa wakinifundisha mimi mifano mizuri, na njia ya Bwana. Nilikuwa Mkristo miaka 3 iliyopita, nilipokiri Yesu na kumkubali awe Bwana na Mwokozi wangu kupitia kwa ndugu/kaka Nicky Cruze . Nilitembea katika njia ya Bwana kwa miaka 2. Lakini nilipoanza High School, nilianza kuasi na kuacha njia ya Bwana. Nilikuwa muasi kwa wazazi wangu na nikajitumbukiza kwenye madawa ya kulevya. Rafiki zangu walinifundisha kufanya mambo hayo. Mimi nilifikiri bado nilikuwa Mkristo, na kwamba naweza kuwaleta marafiki zangu kuwa Wakristo. Lakini badala yake, walinivuta nyuma katika ulimwengu. Ndivyo nikazidi kuwa muasi hata kwa wazazi wangu, na wao walidhani ilikuwa tu kitu cha kwawaida vijana hupitia. Lakini kwa kweli, ilikuwa ni madawa ya kulevya yaliyofanya mimi kufanya hivyo. Roho za uovu ziliingia ndani yangu, ilikuwa ndio wakati mimi nilikuwa muasi kwao. Walikuwa wakali juu yangu, hawakuniruhusu kwenda nje mahali popote, hata kutumia muda wa usiku nikiwa katika nyumba ya rafiki. siku zote nilifanya vitu kwa ujanja au nyuma ya migongo yao. Nilitoroka shule, ilikuwa ni vigumu hata kwenda shule, ilimradi tu kuendeleza tabia yangu. Nilikuwa katika hatua mbaya ya kupata ulevi wa madawa (addiction ), lakini Bwana aliniondoa nje ya yote hayo.




Kama nilivyosema, mimi nilikuwa Mkristo. Ushahidi wangu ulianzia mei 2, 1997. Mimi nilikuwa na rafiki, na tulikuwa marafiki tu, hakuna kitu zaidi ya hapo, naye alijua hivyo pia. Mimi nilifikiri nilikuwa nimemjua, lakini kumbe sikuwa nimejua kwa halisi alikuwa nani. Huo usiku, alinipigia na kuniuliza kama tunaweza kutoka pamoja.Wazazi wangu hawakuwa nyumbani. Walikuwa kwenye mkutano wa maombi, kama kila Ijumaa. Niliwaambia wazazi wang u kuwa nilitaka kukaa nyumbani kwa sababu nilijihisi mgonjwa.

*Imefasiriwa na Peter Kahale kwa Neema aliojaliwa na Mungu*

Mimi nilikuwa ninawadaganya, kwa sababu nilikuwa na mipango ya kwenda nje usiku na rafiki yangu huyo tofauti, lakini wazazi wangu hawakuniachia kwenda kwa rafiki yangu. Hivyo waliniamuru kukaa nyumbani, walipokwenda kwenye mkutano wa Maombi, rafiki yangu alinipi gia. Akaniambia, *"Kwa nini usitoke, kila mtu wakati huu anatoka?"* nilijifikiria mwenyewe.
*"Sitaki kuwa mtukutu kwa wazazi wangu, lakini labda nikitoka kwa ujanja, wazazi wangu wasingekuja kujua kamwe* ", na ndivyo nilivyofanya usiku wazazi wangu waliporudi nyumbani, na kulala usingizi. Nilikuwa tayari kuchoropoka hivyo nilimpigia rafiki yangu na kumwambia anisubirie katika kona ya mtaa wangu. Nilimwambia asipitie nyumbani kwa sababu sauti inaweza kuwaamsha wazazi wangu, na kuharibu kila kitu.
Hivyo nikaweka mito chini ya blanketi na kuruka kupitia dirishani. Ninaishi katika nyumba yenye ghorofa mbili na madirisha yote mawili ya nyumba yangu yana nati inazozishikilia lakini kwa sababu wazazi wangu walikuwa wakiniamini, dirisha langu halikuwa na nati zinazoshikilia, na kwa kuwa ninaishi katika nyumba yenye ghorofa mbili, hivyo nikachukua uaminifu wao kama kigezo cha mimi kuruka kutoka juu na nikatua chini. Bwana alikuwa na mpango na kila kitu kwa sababu ningeweza hata kuvunjika mguu wangu, na hiyo ingeharibu kila kitu ambacho alipanga kwa ajili yangu. Nikatembea kuelekea mtaani, na rafiki yangu alikuwepo tayari akinisubiri.
Nilipoingia kwenye gari niliona vijana watatu na msichana mmoja. Nikajiwazia mwenyewe *sitaenda kufanya chochote, nitakunywa sana na kutumia madawa ya kulevya, na kufurahi sana ila sitaweza kufanya zaidi ya hapo*, lakini nilihofia wanaweza kuchukulia hali yangu hiyo kama nafasi yao kunifanyia chochote. Nikaingia katika gari, kisha tukaondoka. Kabla, wakati nilipokuwa nazungumza na rafiki yangu katika simu, alisema kwamba tutakuwa tukizungukazunguka mji tu. Mimi nikasema *"sawa hiyo inaonekana kuwa safi",* ndio maana nilikwenda. Sikudhania kuwa angenichukua mpaka kweye moteli. Lakini ndipo waliponipeleka, tulipofika walitushusha katika chumba chenye huduma ya kufulia ambacho ni cha moteli hiyo, wakatuambia tuwasubiri pale; wakasema wanakwenda kumchukua rafiki mwingine, nikasema sawa, lakini nilihisi walikwenda kupanga chumba.Waliporudi kutuchukua ,walitupeleka katika hicho chumba. Wakasema, *"msijali, wekeni imani yenu kwetu Sisi hatuta kwenda kufanya chochote!, Tunakwenda kumsubiri rafiki yetu mwingine aje, na kisha tutaondoka wote kwa pamoja* "Kwa hiyo mimi nikaweka imani yangu kwa rafiki zangu, mimi nilidhani kamwe wasingeweza kunidhuru, lakini kwa kweli sikuwa nimefahamu marafiki zangu walikuwa ni watu wa namna gani. Mara ya kwanza, tulikuwa tukizungumza tu, hivyo nikasema, *"wakati sisi tunawasubiri, kwa nini tusipate kitu cha kunywa?* "Hivyo mimi na rafiki yangu tukaondoka mle chumbani, na kutembelea kwenye mgahawa mdogo mbele ya moteli. Tukanunua sprite tatu na kisha tukarudi chumbani. Wakaanza kumimina Sprite katika vikombe. Hawakuleta mfuko au kitu chochote kwamba kinachoonekana kinatuhuma, kwamba kingenifanya niwaze kuwa wanataka kuweka kitu chenye madhara katika kinywaji changu au kunifanyia chochote. ilionekana hakuna hatia yeyote Nilikwenda chooni kurekebisha nywele zangu na kufanya mambo ya kisichana, na nilipotoka kikombe changu kilikuwa tayari kimekwisha hudumiwa

nikaweka jojo (gum) yenye ladha ya strawberry kinywani mwangu, na kuanza kunywa kile nilichofikiri kuwa sprite yangu.
Baada ya hili, sijui nini kilitokea. Lakini nilipopata kuona, nilihisi roho yangu ikitoka nje ya mwili wangu. Nilikuwa tayari katika hospitali; nikaona madaktari na wauguzi wote wamenizunguka karibu yangu. Wakati nilipokuwa nje ya mwili wangu, niliona mwili wangu juu ya kitanda. Wewe unajua jinsi unavyoonekana ukijiangalia katika kioo, unaweza kuona taswira. Lakini ile haikuwa taswira bali, niliona mwili wangu pale juu ya kitanda.

Nilipogeuka nyuma, kulikuwa na watu 2 wamevaa nguo nyekundu, *"wakija tulipo"* wakanishika mimi, mmoja katika kila mkono. Walinipeleka hadi mahali, na wakati nilipoangalia ni wapi ilikuwa ni mbinguni! Kitu cha kwanza kuona tazama ilikuwa ni ukuta mkubwa sana. Ulikuwa ni mweupe na umepanda juu hata usiweze kuona na mwisho wake, katikati ya ukuta ulikuwepo mlango, mlango mrefu, lakini ulikuwa umefungwa.  Katika Agano la Kale, Musa anaongea kwa habari ya hema na anaeleza sifa zake. Nami nilikumbuka hili, na nikaona kuta zake zinafanana na jengo hilo. Pembeni mwa mlango, kulikuwa na kiti kikubwa, na kulikuwa na kiti kidogo katika mkono wa kuume. Navyo vilionekana  vimeundwa kwa dhahabu , na upande wangu mimi wa kuume ulikuwa ni mlango mkubwa mweusi, palionekana ni giza kuzunguka eneo lile lote lakini nilifahamu kwa sababu ya kitasa. Ulikuwa ni mlango mbaya. Upande wangu wa kushoto ilikuwa ni paradiso, kulikuwa na miti, maporomoko ya maji safi ,ilikuwa ni sehehmu nzuri sana yenye amani ila hapakuwa na mtu.
Nikaangalia nikamuona Baba mbele yangu, sikuwa nimeona sura yake, kwa sababu ya utukufu wake, ulikuwa mkubwa, unaangaza sana, uliangaza mbingu yote.Utukufu wake unafanya kila kitu kuangaza. Hakukuwa na jua, mwezi, nyota, yeye ndiye alikuwa mwanga. Niliweza kuona mwili wake, mwili wake ulikuwa pamoja na wa mwana, walikuwa kila mmoja ndani ya mwenzie, walikuwa pamoja, unaweza kuona muachano wa miili yao, lakini walikuwa pamoja kila mmoja ndani ya mwenzie, walikuwa pamoja. Pembeni mwao kulikuwa na malaika wawili Gabrieli na Mikaeli. Sababu ya mimi kujua majina yao ni kwa sababu yaliandikwa kwenye paji la nyuso zao kwa Dhahabu. Nilipokuwa mbele ya Baba, nilijiona mchafu! nilianguka kwa magoti nikaanza kulia. Nilikuwa najionea aibu, Ijapokuwa nilikuwa naweza kuona nyuso zao, sikutaka kuwaangalia, kwa sababu nilijionea aibu mwenyewe kwa jinsi nilivyokuwa mchafu. Nilipokuwa mbele ya Bwana alinionyesha mkanda/picha nzima ya maisha yangu kuanzia mwanzo mpaka sasa. Akaniambia kitu cha msingi ni vile ambavyo nilifanya baada ya kuokoka. Nilikuwa nawaambia marafiki zangu kuwa mimi ni mkristo, lakini kiukweli sikuwa naonyesha matunda yangu. Akaniambia kuwa ilinipasa niende kuzimu. Malaika Gabriel akaja na akanishika katika mkono wangu. Akanipeleka katika mlango ule mweusi mbaya ambao nilikuwa sitaki hata kuuangalia. Nilijitahidi kujizuia, lakini nilikuwa katika roho, na tukapita mlangoni, nilipokuwa upande mwingine wa mlango, ilikuwa ni giza kila upande. Sikuweza hata kujiona mwenyewe. Kisha tukaanza kuanguka Haraka sana kama wimbi la ufukweni (roller coaster).Nilipokuwa nikidondoka chini palikuwa panazidi kuwa na joto zaidi. Nikafunga macho yangu; Sikutaka kuona mahali tulipokuwa.

Tulipoacha kudondoka, nilifungua macho yangu, na nilikuwa nimesimama kwenye barabara kubwa. Sikuwa nimefahamu inaelekea wapi, lakini kitu cha kwanza ambacho nilihisi ilikuwa na kiu. Nilikuwa na kiu sana! Nikawa naendelea kumsisitiza malaika *"ninakiu, ninakiu"* Lakini ilikuwa ni kama hakuwa ananisikia. Nikaanza kulia, na machozi yangu yalipodondoka chini kwenye mashavu yangu, yalipotea kabisa kama mvuke. Kulikuwa na harufu ya Sulphur, kama tairi ikichomwa. Nilijitahidi kuziba pua , lakini hiyo ndiyo iliongeza harufu. Hisia zangu zote tano zilifanya kazi kwa nguvu sana. Nilipokuwa najitahidi kujifunika mwenyewe, ndivyo nilivyozidi kunusa harufu ya sulfur zaidi. Pia, vinyweleo vyangu katika mikono vilipotea. Nilihisi joto lote, kulikuwa na joto sana.
Nilipoanza kutazama mahali pale, Niliona watu wakiteswa vibaya sana na mapepo. Kulikuwa na msichana pale anaumia sana, pepo lilikuwa likimtesa. Hili pepo lilikuwa likimkata kichwa chake kwa mkuki mrefu, na likimchomachoma kila sehemu. Halikujali. Kwenye macho, kwenye mwili, kwenye mikono, halikujali. kisha linarudisha kichwa chake tena na kumchoma kila sehemu. Alikuwa akilia kwa sauti ya kilio kikuu cha huzuni.

Kisha tena nikaona pepo jingine, hili pepo lilikuwa likimtesa kijana wa kiume mdogo mwenye umri kati ya miaka 21-23. Huyu kijana alikuwa na mnyororo kwenye shingo yake, na alikuwa amesimama mbele ya shimo lenye moto. Hili pepo lilimchoma kwa mkuki mrefu kila sehemu ya mwili wake, kwenye macho, kila sehemu. Kisha pepo linamvuta kwa nywele zake kijana na kwa mnyororo wake na kumtupia shimoni, kisha linamchukua tena na kuanza kumtesa na kumtesa. Hii iliendelea hivi wakati wote, na kila alipokuwa akiingia ndani ya shimo hilo, nilikuwa sisikii kilio chake, Lakini pepo lilipokuwa likimtoa mle shimoni ndipo nilisikia kilio kikuu sana cha uchungu. Nilijitahidi kuziba masikio yangu kwa sababu sauti ilikuwa inaogopesha sana, lakini nilikuwa namsikia. Masikio yangu yalikuwa na nguvu ya kusikia zaidi.

Niliangalia pepo jingine, hili pepo lilikuwa ni baya, na mengine yale mawili yalikuwa mabaya lakini hili lilikuwa baya zaidi ya yale mengine. Mfano wake lilikuwa na sura na tabia ya wanyama mbalimbali; siwezi hata kusimulia kwa maneno. Lilikuwa likizunguka na kuwatishia watu, na watu walikuwa wakiogopa sana. Kisha nikaona pepo jingine, lakini hili pepo lilikuwa lina sura nzuri kama ya malaika wa Mungu, lakini sivyo.Tofauti niliyoiona kati ya malaika wa Mungu na mapepo ni kuwa mapepo hayakuwa na majina yaliyoandikwa katika paji ya nyuso zao kwa dhahabu, lakini malaika wa Mungu walikuwa na majina katika nyuso.

Kisha nikamuangalia malaika Gabrieli, na alikuwa akiangalia juu. Nadhani alikuwa hapendi kuona wengine wanavyoteswa. Nikafikiri moyoni mwangu, *"kwa nini bado yuko mahali hapa? Je , sitakiwi kuwepo mahali hapa na kusubiri zamu yangu ya kuteswa?* Nilikuwa na kiu. Nikalia kwa malaika, *"Nina kiu, nina kiu,"* Nafikiri alinisikia kwa sababu alitazama chini na kuniangalia akasema, *"Bwana anakwenda kukupa nafasi moja nyingine."*

Mara aliposema hivyo, kiu yangu yote ikaondoka, uchungu wangu, maumivu yangu, yote yakaondoka . Nikajihisi nina amani. Kisha akauchukua mkono wangu, tulikuwa karibu na kuondoka, Kisha nikasikia sauti yangu ikiitwa , "Jennifer, Nisaidie mimi, nisaidie !" Niliangalia

chini. Nilihitaji kujua alikuwa ni nani, Lakini nilipojaribu moto uliwaziba sura zao sikuweza kuwajua. Ilikuwa ni sauti ya msichana. Niliweza kuona mikono yake ikiwa imetokeza, alitaka nimsaidie. Nilikuwa natamani kumsaidia kweli, Nilipojaribu, nilishindwa , kwa sababu mikono yangu haikuweza kumshika, Nilitaka kumsaidia kabisa lakini unaweza kuona hakuwa na matumaini tena. Sikuweza kumsaidia.

Na kisha nikaangalia kote nikaona rafiki zangu, watu ninao wafahamu, na watu wengine. Walionekana kama ninawafahamu lakini sikuweza kuwatambua walikuwa ni akina nani. Sikufahamu maisha yao, lakini nilipowaona marafiki zangu wa shuleni pale, iliniumiza sana!. Nikajiwazia mimi mwenyewe, *''Labda kwa sababu ya ushuhuda mbovu niliowaonyesha, wa kusema kuwa nilikuwa mkristo lakini nikarudi nyuma, ndicho kilichowafanya nao wasipende kumjua Mungu, na wakaamua kumuacha. Labda ilikuwa ni mimi niliyewaleta pale''.*Hivyo ndivyo nilifikiri. Niliona katika kuzimu hakuna muda, hakuna wakati uliopita, wakati wa sasa, wakati ujao, kila kitu ni vile vile, na imewapasa kwenda pale. Lakini kama nilivyosema mwanzoni sipendi kuweka msingi wowote, Lakini hicho ndicho nilichokiona. Watu niliowaona pale bado wanaishi hivi leo.

Malaika akanichukua tena na kunipeleka katika uwepo wa Mungu. Nilipokuwa nimesimama mbele zake, nilipiga magoti kisha nikaanza kulia na kulia. Nilikuwa bado siwezi kumtazama kwenye uso wake, kwa sababu nilikuwa ni mwenye kujionea haya. Lakini Yesu pamoja na sauti yake hiyo nzuri akasema, *''Nakupenda''* Upendo wake ni kama wa haki, Nawapenda wanaonisikia mimi. Lakini akaniambia amenisamehe makosa yangu yote nilipokuwa nimemuasi. Alinisamehe.

Mungu akaniangalia kisha akanionyesha mambo mengi yajayo. Akanionyesha Ulimwengu yaani dunia. Kuzunguka Dunia niliona kitu kama kilaini, kama tabaka la ozone, lilikuwa limezunguka ulimwengu mzima, lilikuwa ni laini sana, nilitamani hata kushika. Niliposhika nilijua alikuwa ni Roho Mtakatifu, kwa sababu ilinibatiza na kuanza kuongea kwa lugha nyingine.

Wakati huo, Nilitazama juu na kuona roho chafu nyingi zikitoka nje yangu. Nilipokuwa nikijiachia na kutumia madawa, ambayo yaliingia mpaka kwenye fikra zangu na kuruhusu mlango, wa roho hizi chafu kuja na kukaa ndani yangu. Roho hizi chafu zilinitesa. Kiasi kwamba nilivyokuwa nikifanya haikuwa ni mimi halisi, ilikuwa ni zile roho chafu ndani yangu. Neno la Mungu linasema kwamba nyumba yako inapokuwa imesafishwa roho chafu zitajaribu kuja tena kwa kuleta wengine 7. Nyumba yangu ilisafishwa mara nilipokuwa nimeokoka. Na niliziona hizi roho chafu nilipokuwa nikibatizwa na Roho mtakatifu, walikuwa wako 7, na hizo 7 zilikuwa na wengine 7, na sikuweza hata kuzihesabu zote! Lakini Bwana alinisafisha na roho zote chafu.

Pia alinionyesha kwa habari ya mambo yajayo, akanionyesha Dunia na mambo ambayo yatakuja kutokea, matukio yakakayokuja kutukia. Maono niliyopewa ni kuanzia sasa mpaka wakati wa unyakuo. Hakunionyesha unyakuo, lakini alinionyesha mambo yatakayotokea kabla ya unyakuo. Kila siku ilisogea kidigokidogo, na ninakuambia kuwa unyakuo umekaribia! Unatakiwa

kujichunguza mwenyewe, maisha yako, na kujiuliza “ *Je niko tayari kwenda na Bwana?*” Bwana alinionyesha hili, lakini aliniambia nisimueleze mtu yeyote, lakini kusubiri na kuona kuwa mwisho umekaribia, sipendi nimjaribu Mungu, ndio maana sitapenda kuwaambia kile nilicho kiona. Lakini nawaeleza na kuwatahadharisha kuwa unyakuo umekaribia.

Ninasoma katika Joel 2:28, ni moja kati ya unabii wa mwisho; kila kitu kingine kimekwisha timia. Unabii huu ndio wenyewe tu ambao haujatimia na ninakueleza wewe kuwa unabii huu unaendelea kutimia, Vijana wengi hivi sasa wanatokeza na kuhubiri neno la Mungu. Shetani anataka kufanya jeshi la vijana lakini Bwana atakuwa na nguvu zaidi yake. Na kama kweli ukimkubali na ukipenda kumtumikia, Bwana atakupa uwezo wa kumshinda shetani, ili ukahubiri neno la Mungu Ulimwengu wote, Kama jinsi alivyoamuru katika Biblia.

Aliniambia mimi kuwa nina mpango, na mpango huu ni kuwaeleza vijana wote kuhusu maono yangu. Hata kama sitataka kufanya hivi, ni amri ambayo Mungu alinipa, na nitaimaliza.

Niliporudia mwili wangu, niliamka na kujikuta nikiwa hospitali.Niliangalia huku na huko na kuona sindano katika mikono yangu,vitu vikiangalia moyo wangu, mashine. Mara wazazi wangu wakaingia ndani nikaanza kulia. Walionekana ni wenye ghadhabu, lakini Bwana akaniambia niwaeleze kila kitu na hicho ndicho nilichofanya. Niliwaeleza kila kitu.

Nesi alipoingia ndani ya chumba, wakanieleza kuwa walikuwa wanahofia sana kwa habari yangu. walisema nilikuwa naondoka na kurudi. Nilikuwa sijitambui halafu mara najitambua tena. Hii ilitokea mara tatu. Wanasema kuna wakati fulani katika matukio hayo matatu sikutaka kurudi kabisa, wakawa na hofu sana kwa habari yangu. Wanasema moshi ulikuwa ukitoka katika kinywa changu na kutoa maneno yasoyoweza kueleweka.

Pia usiku ule, mama yangu alikuwa na ndoto mbaya. Kimbwa kidogo ambacho nilikuwa nikilala nacho kilikwenda kwenye chumba cha wazazi wangu na kukwarua mikono ya mama yangu na kujaribu kumuamsha. Alipoamka, alikwenda kwenye chumba changu na kuona mito ikiwa imewekwa vizuri na kufunikwa. Akafikiri nilikuwepo akarudi tena kwenye chumba chake. Kisha akaangalia dirishani akaona taa za polisi nje ya dirisha zikimulika. Alipochungulia dirishani, akaona polisi wakija kwenye Nyumba yetu, hivyo akamuamsha baba yangu. Polisi akawaambia wapige simu kituo cha polisi ili kupata taarifa zaidi kuhusu mimi. Wazazi wangu ndipo walipofahamu kuwa nimedhurika zaidi na sumu na kwamba niko hospitalini. Wakati huo Bwana akaongea na baba yangu na kumwambia asiogope, Nilitumia muda wa siku tatu nikiwa hospitali.

Wiki moja baadae tuliongea na maaskari, na wakatusimulia kwa habari ya usiku ule. Wakasema Yule msichana niliyekuwa nae , hakutakiwa kutoka nje pia, na baba yake aliogopa sana. akawa akimtafuta, akizunguka , lakini hakuweza kumuona. Hivyo akaenda katika kituo cha polisi, na akatangaza aina ya gari ambayo rafiki yangu alikuwa akiendesha kwa wote wanaofanya patrol. Afisa fulani aliyekuwa hayuko kwenye zamu, alikuwa akipita mtaani kuzungukia wauzaji wa magari, alikuwa akitafuta gari ya kununua iliyotumika. Akawa ameona gari ya rafiki yangu akawa amewaita polisi. Polisi walipokwenda kuchunguza, gari ya rafiki yangu ilikuwa

imeegesha mahali pengine, hivyo hawakujua mahali gani alikuwepo binti huyo.Tulikuwa kwenye ghorofa ya pili katika chumba kilicho kwenye kona. Polisi walitaka kuanza kukagua katika chumba kile, na washuke chini wakimuuliza kila mmoja ni nani mwenye gari ile iliyopaki pale nje. Walikuwa hawamtafuti Yule msichana; walikuwa wakimtafuta mmiliki wa gari ile.

Walipogonga mlangoni petu, walifungua mlango na kuniona mimi niko chini.Lakini wakaondoka. Niliowaita rafiki zangu walidhani kuwa Polisi wameondoka tu , kumbe waliondoka kuchukua gari ya wagonjwa Ambulance. Mara tu polisi wengine wakaingia ili kuona nini kinaen delea.Walipofungua mlango, muda ule sasa, rafiki yangu yule niliyekuwa nikimuongelea, Yule niliyemuamini alikuwa katika pointi ya kunibaka. Lakini Bwana akatumia polisi ili kuzuia kitendo kile, na hawakunifanya chochote. Hicho ndicho nacho mshukuru Bwana, kwa kuwa alikuwa mwenye Rehema kwangu.

Na maombi ya wazazi wangu, naongea na nyie wazazi. Msiache kamwe kuomba kwa ajili ya watoto wenu. kama hawatembei katika njia ya Bwana, endeleeni kuwaombea, msikate tamaa. Wazazi wangu hawakukata tamaa, na angalia mahali nilipo hivi sasa, ninahubiri neno la Mungu; nikiwaambia vijana waje kumtumikia Mungu, kwa sababu wanamuhitaji.

Ningependa kutoa ujumbe kwa vijana wote, ningependa wewe uwaze kwa habari yako, na ujichunguze mwenyewe. Fikiria, kwa nini ujali kile mtu yeyote anasema kwa ajili yako wewe. Nimekuwa nikifikiri kile Watu wamekuwa wakisema kwa habari yangu mimi lakini sasa nimegundua hata hawanijali. Hawatakuwa pale Bwana atakapokuwa mbele yangu. Nakumbuka nilipokuwa mbele ya Bwana, marafiki zangu hawakuwepo pale kunisaidia,familia yangu haikuwepo pale kunisaidia,mchungaji wangu hakuwepo pale kunisaidia,kanisa halikuwepo pale kunisaidia. Nilikuwepo pale peke yangu, na nilihitajika kujitetea mwenyewe.Mbele zake huwezi kuona uongo, kwa sababu ni mtakatifu sana. Na nilipokuwa pale, sikujisikia kuwa mimi ni wa pale, kwa sababu nilikuwa katika dhambi na mbinguni ni patakatifu.

Ninakueleza wewe hivi leo kama haujampokea Bwana Yesu, basi mpokee hivi leo.Huu ni uamuzi wa Busara sana katika maisha yako yote. Sikuelezi haya yote ili kuwaogopesha ili muingie mbinguni, lakini ili muweze kuona rehema, upendo alionao kwetu sisi. Yeye Baba, alimtuma mwanae wa pekee afe kwa ajili yetu. Hivyo kila tone la damu alilomwaga linasafisha dhambi zetu zote. Kama unataka kumpokea Bwana, ni uamuzi muhimu sana katika maisha yako. Njoo kwa Bwana, Usijali nini kile mtu mwingine anasema kwa habari yako.

Kama unataka kumtumikia Bwana ,basi fanya kwa moyo wako wote , usiiseme tu kwa mdomo wako,sema kwa moyo wako na fikra zako.Usihofu kwa habari ya maisha ya baadae,usihofu kwa ajili ya leo, huwezi jua ni lini utakwenda kufa. Nina umri wa miaka 15 tu na katika fikra zangu sikuwa nimewaza kuwa nitakufa katika umri wa miaka 15, sikuwahi kuwaza hivi.

Unatakiwa kufikiri pia kuhusu hilo. Maisha yangu si yangu,maisha yako si yako,tumekopa maisha yetu, maisha yetu ni ya Mungu. Huwa tunapuuzia sana kuhusu hili na hatujali, tunarudi katika ulimwengu, na kufanya mambo ya ulimwengu. Ulimwengu una mambo mengi ya kukupa,

lakini kumbuka Mungu anamambo mengi pia ya kukupa. Ulimwengu una kuzimu na mauti, lakini Mungu anao uzima wa milele. Maisha ya milele ni milele.

Hivi sasa kama unataka kumkubali Bwana, Ninataka uinamishe kichwa chako na kufunga macho yako, nifuatishe maneno haya *"Bwana Mungu, katika jina la Yesu, nakuja kwako leo, O Bwana Mungu wangu kwa wakati huu nakukubali Wewe kama Mwokozi wangu, nataka uje katika maisha yangu. Kama dada alivyosema kuhusu ushahidi wake kwamba Kuzimu ni halisi, yeye alikuwa huko. Bwana Mungu, sitaki kwenda huko, sitaki hata kufikiri kwa habari ya kwenda huko. Bwana Mungu ninaomba unisamehe dhambi zangu zote nilizozifanya. Nisamehe kwa kila kitu ambacho nimekuwa nikifanya. Kila dhambi ndogo ya siri, Bwana Mungu wangu, mimi nazitangaza mbele yako, hivyo tafadhali nisamehe kwa kila kitu. Bwana Mungu naamini kwamba Wewe alikufa msalabani na kwamba ulifufuka kutoka katika wafu. Naamini kwamba utakuja moyoni mwangu na kutawala moyo wangu, na kuwa moyoni wangu. Nitasoma neno lako, na nitakuwa zaidi katika Neno. Nitakwenda Kanisani, Bwana Mungu wangu kwa sababu mimi najua Wewe unapatikana pale Kanisani. wewe umesema kwamba watu wawili au watatu wakikusanyika pamoja, Wewe hukokatikati yao. Bwana, Mungu wangu nataka kuwepo ambapo Wewe upo. Naomba haya yote katika jina la Yesu, Amina* "

Kama umeomba sala hii, ningependa kukukaribisha katika ufalme wa Mbinguni. Sasa una ndugu kaka na dada zako ulimwengu mzima. Hii ndio uamuzi wa muhimu sana katika maisha yako kati ya maamuzi ambayo ulishawahi kufanya , hivyo usipuuzie. Usirudi tena kwenye ulimwengu. Ulimwengu unakuongoza kwenye mauti, lakini Mungu anatuongoza kwenye uzima wa milele.Kila muda imekupasa uishi kana kwamba ni siku ya mwisho, na siku yako ya mwisho. Kama ushuhuda huu umegusa moyo wako, mpe pia rafiki yako ili kwamba amkubali Mungu katika moyo wake. Usiruhusu muda huu ukupite, huu unaweza kuwa ndio wakati wako wa mwisho.

## Kuzimu ni halisi, nilikwenda huko!

na ***Jennifer Perez***

*Ndugu aliyefasiri ufunuo huu ni Peter Kahale ni kijana aliyeokoka na anampenda Yesu na mwenye shauku ya kuhubiri injili ya Yesu Kristo.*
*Simu ya Mkononi: +255-769-610460, +255-653-610460.*
*Barua Pepe: kahalepeter@gmail.com.*

*Imefasiriwa na Peter Kahale kwa Neema aliojaliwa na Mungu*